

PreK 4 ME, Uhusiano wa Familia


# SOMO LA 1: *FAMILIA*

## ***Muhtasari wa Somo la 1: Familia***

*Masomo yetu mwezi huu yanaangazia familia za wanafunzi wetu, na jinsi wanafamilia wanavyohusiana na kusaidiana. Kupitia masomo haya, tutachunguza jinsi familia zinavyoshirikiana kutatua shida, mizozo na changamoto, na kuhusu wajibu na majukumu mengi ndani ya familia. Pia tunajitahidi kujifunza stadi za msingi za herufi na sauti zinazotoa. Tunakagua mitazamo tofauti ya wanafunzi wenzetu na jinsi ya kutatua shida zinazotokea darasani mwetu.*

*Endelea kusoma uone kile kinachotokea katika darasa letu la PreK na uwawezeshe watoto wako kujifunza pamoja na sisi!*

### VITABU VYA SPOTLIGHT vya Somo la 1





*Peter's Chair*

Cha Ezra Jack Keates





*The Hello, Goodbye Window*

Cha Norton Juster na Chris Raschka




*Time for Bed*

Cha Mem Fox




*Families*

Cha Shelley Rotner na Sheila M. Kelly

Picha zimetolewa Amazon.com

### Vitabu vingine tunavyosoma:

*Cry Baby* cha: Karen Beaumont

*Sometimes I am Bambaloo* cha: Rachel Vail

*Corduroy* cha: Don Freeman

*A Pig is Big* cha: Douglas Florian

*Viatu, Viatu, Viatu* cha: Ann Morris

## Nyimbo, Herufi na Michezo ya Lugha

Sasa tunawaletea mafunzo wanafunzi wetu kupitia mazoezi ya kufurahisha ya makundi. Tunaanza kuhesabu… vyura:

### Vyura Watano Wekundu

**Vyura watano wekundu, wameketi kwenye jiwe kubwa wakila vidudu vitamu... TAM! TAM!!**

**Mmoja ameruka na kutumbukia ndani ya bwawa lenye maji moto mazuri, sasa wamebakia vyura wanne wekundu... NAAM! NAAM!**

**Vyura wanne wekundu, wameketi kwenye jiwe kubwa, wakila vidudu vitatu... TAM! TAM!!**

**Mmoja ameruka na kutumbukia ndani ya bwawa, lenye maji moto mazuri, sasa wamebakia vyura watatu wekundu... NAAM! NAAM!**

**Vyura watatu wekundu, wameketi kwenye jiwe kubwa, wakila vidudu vitamu.. TAM! TAM!!**

**Mmoja ameruka na kutumbukia ndani ya bwawa, lenye maji moto mazuri, sasa wamebakia vyura wawili wekundu... NAAM! NAAM!**

**Vyura wawili wekundu, wameketi kwenye jiwe kubwa, wakila vidudu vitamu.. TAM! TAM!!**

**Mmoja ameruka na kutumbukia ndani ya bwawa, lenye maji moto mazuri, sasa amebakia chura mmoja mwekundu... NAAM! NAAM!**

**Chura mmoja mwekundu, ameketi kwenye jiwe kubwa, akila vidudu vitamu... TAM! TAM!!**

**Mmoja ameruka na kutumbukia ndani ya bwawa, lenye maji moto mazuri, sasa hakuna vyura (0) wekundu waliobakia... NAAM! NAAM!**

***Angalia sehemu inayofuata uone mazoezi ya nyumbani***

# Wezesha Masomo ya Nyumbani Kupitia Mazoezi haya ya Ziada

| Zoezi hili linatimiza viwango vyetu vya Lugha, Mahusiano ya Kihisia na Kijamii | Zoezi hili linatimiza viwango vyetu vya Ujuzi wa Kusoma na Ubunifu wa Kisanaa | Zoezi hili linatimiza viwango vyetu vya Hisabati |
|---|---|---|
| **Picha za Familia** | **Linaanzia Na** | **Zoezi la Hisabati** |
| Ikiwa una albamu za picha za familia—ziangalie pamoja na mtoto wako. Ongea kuhusu watu walio kwenye picha, mahusiano na kumbukumbu. | Mwambie mtoto wako atafute vitu vitatu karibu na nyumba ambavyo vinaanzia na sauti sawa na jina lake, na umwambie achore picha za vitu hivyo. | Tufanye zoezi la Hisabati! Msaidie mtoto wako kutafuta vitu 2 au 3 karibu na nyumba ambavyo ni vya idadi sawa (kalamu mbili, vifuniko viwili, nk.). Mwambie mtoto wako avipange au kuviambatisha kwa gundi kwenye karatasi. Mwambie avihesabu. |

***Vidokezo vya Kipindi cha Kumsimulia hadithi mtoto wako:***

⇒ Tafuta mahali pazuri pa kuvutia, ambapo hamtasumbuliwa

⇒ Unaposoma, mwonyeshe mtoto wako maneno kwa kuyafuatilia kwa kidole

⇒ Fafanua msamiati mpya au maneno magumu unapoendelea kusoma



Picha imetolewa Pixabay

Ushauri kwa Watunzaji na Familia zetu:

Katika hatua zote za ukuaji wa mtoto wako, ni muhimu kufuatilia shughuli zake za kujifunza siku nzima. Kwa wazazi wanaofanya kazi, mara nyingi ni vigumu kufanya hivi lakini hurahisishwa kwa kuwasiliana kwa uwazi na wale wanaomtunza na kumsomesha mtoto wako. Hakikisha mlezi wako amesasisha maelezo kuhusu jinsi ya kuwasiliana nawe. Ongea na mlezi mara nyingi iwezekanavyo, hata kila siku, ili ujue kile mtoto wako anajifunza na jinsi anavyoendelea. Unga mkono masomo ya shule ya chekechea au kituo cha malezi kwa shughuli ambazo wewe na mtoto wako hufanya nyumbani. Aina hii ya mawasiliano na walezi na walimu itamsaidia mtoto wako kukua kimasomo, kijamii na kihisia, na kumwezesha mtoto wako kupendana na wewe zaidi.

Kumbuka kuwa kila aina ya mwingiliano na mtoto wako ni nafasi ya kujifunza na kwamba atajifunza katika maeneo mengine mengi kando na shule.

Chanzo: https://eclkc.ohs.acf.hhs.gov/parenting/article/you-your-preschool-child#Needs